BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAJUMUISHO YA MIJADALA YA BAJETI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai na kutuwezesha kukutana tena leo hii, tukiwa wazima wa afya ili kutekeleza wajibu wetu wa kuwatumikia wananchi. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii adhimu kwa niaba ya Kamati yangu ya Bajeti ili niweze kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Hotuba ya Kamati ya Bajeti kuhusu Majumuisho ya Mijadala ya Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Nakushukuru pia Mheshimiwa Spika, wewe pamoja na wasaidizi wako wote kwa namna mnavyoliongoza vyema na kwa weledi Baraza hili hali ambayo inatuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake mahiri na juhudi zake za kuiletea maendeleo ya haraka nchi yetu. Mafanikio tunayoyaona sasa ni matokeo ya ushirikiano mzuri anaoupata kutoka kwa wasaidizi wake, Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais, na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais. Kwa

dhati kabisa, tunawapongeza wote kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipekee na kwa dhati kabisa, naomba kutoa shukrani nyingi kwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano yao kwangu binafsi, Makatibu wetu wa Kamati, na kwa umakini wao wakati wote ambao Kamati imekuwa ikifanya kazi zake. Maoni na ushauri wao umekuwa msingi muhimu katika kuandaa Hotuba hii ninayoiwasilisha muda huu. Ili kuzipa uzito shukurani zangu kwao, naomba uniruhusu niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdalla Mussa Mjumbe
4. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha Mjumbe
5. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad Mjumbe
6. Mhe. Rukia Omar Ramadhan Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Masoud Makame Mjumbe
8. Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kuwashukuru Makatibu wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wao kwetu na uratibu mzuri wa shughuli za Kamati, naomba pia kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:

1. Ndg. Abass Vuai Moh'd Katibu
2. Ndg. Asha Said Mohamed Katibu
3. Ndg. Husna Rajab Othman Katibu
4. Ndg. Shaib Fadhil Shaib Katibu

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa hotuba hii, ni matakwa ya Kanuni ya 113(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2024 ambayo inaielekeza Kamati ya Bajeti kwa kushirikiana na Serikali kufanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya mashauriano hayo na kwa kuzingatia Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2024 ambayo inanipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Baraza Hotuba ya Majumuisho kabla ya kuwasilishwa Mwelekeo wa Mpango wa Taifa na Makadirio ya Bajeti ya Serikali. Aidha, kutokana na umuhimu wa utekelezaji wa hoja zilizochangiwa na kusisitizwa na Wajumbe wengi, Kamati imeona ni vyema kuzikumbushia hoja hizo sambamba na kuishauri Serikali ili kuhakikisha utekelezaji wa bajeti za Wizara unafanyika kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## UFAFANUZI WA HOJA ZILIZOJADILIWA WAKATI WA KIKAO CHA MAJUMUISHO BAINA YA KAMATI YA BAJETI NA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao cha majumuisho kati ya Kamati ya Bajeti na Wizara ambazo baadhi ya hoja zake ambazo zilihitaji ufafanuzi wa ziada baada ya mchakato wa kupitishwa bajeti za Wizara hizo na hivyo kujadiliwa tena katika Kamati. Jumla ya hoja mbili (2) kutoka katika Wizara mbili (2) zifuatazo zilizojadiliwa:

i. Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (OMPR)
ii. Wizara ya Afya (WA)

**Mheshimiwa Spika**, Kwa lengo la kurahisisha ufafanuzi wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati ya Bajeti kwa kushirikiana na Wizara husika, tumeziweka katika mfumo wa Jadweli ambalo limegawika katika Sehemu Tatu; **Sehemu ya Kwanza** inahusu Hoja Zilizoibuka, **Sehemu ya Pili** inahusu Majibu ya Wizara na **Sehemu ya Tatu** ni Maoni na Ushauri wa Kamati

JADWELI: HOJA ZILIZOIBUKA

| OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS (OMPR) | | | |
|---|---|---|---|
| Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (OMPR) | | | |
| SNo. | HOJA ZILIZOIBUKA | MAJIBU YA WIZARA | MAONI YA KAMATI |
| 1. | Fedha za Mfuko wa Jimbo kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) kiasi cha TZS 4 bilioni zimeonyeshwa kama mapato ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ilhali ni fedha za miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa taratibu, mapato yote yanayokusanywa na Ofisi yanapaswa kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, lakini fedha hizi hazijapelekwa huko. Kamati inaomba kupatiwa ufafanuzi kuhusiana na fedha hizi. | Hapo awali Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa Wabunge kwa upande wa Zanzibar zilikuwa zikipokelewa kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina wa SMZ na kuingizwa katika hesabu ya Deposit ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, na baadae kupelekwa katika hesabu za majimbo. Kwa sasa, mfumo wetu mpya wa BAMAS hauruhusu kupokea fedha bila ya kuwa na kifungu cha mapato kwa ajili ya upokeaji wa fedha husika. Hivyo, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango imeanzisha kifungu cha mapato kwa ajili ya kuzipokea fedha hizo, na kifungu hicho kwa mwaka huu | Kwa kuwa fedha zote zinazotoka nje ya Zanzibar zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina, Kamati inashauri kuendelezwa utaratibu huu kwa fedha za Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo kutoka SMT kuingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina halafu ndio zihamishiwe kwenda katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hatua hii itasaidia kuondosha changamoto iliyojitokeza na pia kuipa fursa Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango kupata taarifa sahihi ya kiasi cha fedha zote zilizoingia Zanzibar |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kimeamuliwa kuwekwa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. | kutoka nje. |
| WIZARA YA AFYA (WA) | | | |
| SNo. | HOJA ZILIZOIBUKA | MAJIBU YA WIZARA | MAONI YA KAMATI |
| 1 | Makadirio ya makusanyo ya mapato ya Wizara ya Afya (WA) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yalikuwa TZS 3.72 bilioni na kwa upande wa mwaka wa fedha 2025/2026 imekadiriwa kukusanya TZS 7.023 bilioni. Hii inafanya kuwepo na ongezeko la asilimia 89. Kwa kuwa Wizara ya Afya (WA) ni taasisi ya kutoa huduma na sio taasisi ya kibiashara, ni ipi misingi ya kufanya makadirio hayo ni ipi, na je jambo hili halitaathiri utekelezaji wa majukumu ya | Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Afya Fungu (H01) imekadiriwa kukusanya TZS 7,023,306,000. Aidha, fungu hili kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 3,719,683,000. Ongezeko hilo, linatokana na kuhamishiwa kwa huduma za haraka (Fast Track) kutoka Hospitali ya Mnazi mmoja kwenda Hospitali ya Lumumba. Sambamba na hilo, kuwepo kwa huduma za haraka katika Hospitali za Wilaya na Huduma za Afya kwa Wagonjwa wa Bima ambazo zimepelekea kuongezeka kwa makadirio ya makusanyo hayo kwa asilimia 88. | Kamati imeridhishwa na ufafanuzi uliotolewa. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba ongezeko hili la lengo la ukusanyaji wa mapato yake haliathiri utoaji wa huduma kwa wananchi. Wizara izingatie katika kuimarisha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato badala ya kuongeza gharama za huduma. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Wizara? | | |

## MAENEO AMBAYO YALICHANGIWA NA WAJUMBE WENGI

**Mheshimiwa Spika,** Katika mchakato wa kujadili bajeti za Wizara, kuna baadhi ya maeneo yalichangiwa na Wajumbe wengi zaidi na baadhi yake yalichangiwa kwa hisia na msisitizo mkubwa. Kwa madhumuni ya kuikumbusha Serikali ili kuichukulia michango hii kwa uzito maalum, na kwa kuwa hii ni hotuba ya majumuisho, Kamati yangu imeona ni vyema kuchukua fursa hii kuyachambua na kuyataja maeneo hayo kwa muhtasari ili Serikali iweze kuyafanyia kazi kwa haraka iwezekavyo na hatimae kufikia malengo ya kupata ufanisi katika utekelezaji wa bajeti zetu sambamba na kutoa huduma bora kwa wananchi. Maeneo hayo ni kama yafuatayo:

### Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa bajeti ya Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa RaisWajumbe wengi walitoa michango yao kwa msisitizo mkubwa kuhusu suala la fedha za mfuko wa jimbo kutoendana na mahitaji halisi ya utekelezaji wa miradi katika majimbo. Wajumbe wamependekeza kiwango cha fedha za mfuko wa jimbo kiongezwe na kufikia TZS 30 milioni badala ya TZS 20 milioni ya sasa. Hatua hiyo itasaidia angalau kuhimili ongezeko la gharama za vifaa na huduma za ujenzi. Kamati inaunga mkono mapendekezo haya kwa kuwa yanaendana na uhalisia wa mazingira ya sasa ya kiuchumi na mahitaji katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya majimboni.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la maafa nalo limepewa uzito na Wajumbe wengi, ambapo walisisitiza umuhimu wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kufanya tathmini ya kina katika maeneo yanayoathiriwa na majanga mbali mbali. Maeneo hayo ni pamoja na yale ya makaazi ya watu yanayokumbwa na mafuriko pamoja na maeneo ya pwani ambapo wananchi hutumia bahari kwa shughuli za kiuchumi, usafiri na

mengineyo, na hivyo kuwa katika hatari ya maafa ya baharini. Vilevile, Wajumbe walitoa rai kwa Kamisheni hiyo kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu njia bora za kujikinga na maafa, pamoja na mbinu za uokozi wakati maafa yanapotokea. Kwa kuzingatia kuwa maafa huweza kutokea wakati wowote, Kamati inaunga mkono mapendekezo haya na inashauri Serikali kuhakikisha kuwa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Kamisheni hiyo inatolewa kwa wakati ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

## Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Suala la utunzaji wa mazingira na namna ya kujiepusha na vitendo vinavyochangia uharibifu wa mazingira hayo ikiwemo uchimbaji wa mawe, mchanga na utupaji wa taka ovyo ikiwemo "pampers" ni miongoni mwa mambo yaliyosisitizwa sana Wajumbe wakati wa mjadala wa bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Kwa kuwa, kutunza mazingira ni jukumu la kila mtu, Kamati inatoa wito kwa jamii kuchukua jitihada za kutunza mazingira yetu ili maeneo yetu yawe salama nay a kupendeza. Aidha, Kamati inaishauri Serikali, kuipa kipaumbele miradi ya kulinda mazingira ambayo itasaidia katika kupata afya bora kwa jamii na kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama za matibabu yanayotokana na maradhi yanayosababishwa na uchafuzi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Wajumbe wengi walichangia kwa msisitizo katika Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ni suala la Mamlaka ya Udhibiti wa Kupambana na Dawa za Kulevya kuingiziwa fedha kwa mujibu wa bajeti yao ili Mamlaka iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika kipindi cha Julai – Machi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mamlaka hii ilipata asilimia 5 tu ya makadirio ya mwaka. Upungufu huu mkubwa wa fedha umeathiri kwa kiwango kikubwa

utekelezaji wa majukumu muhimu ya Mamlaka katika mapambano dhidi ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Kutokana na umuhimu wa suala mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mamlaka hiyo zinatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu, ili kuiwezesha kutekeleza kwa ufanisi shughuli zake za udhibiti, uzuiaji na uelimishaji wa umma dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Ifahamike kwamba, matumizi ya dawa za kulevya kunadhoofisha afya ya mtuamiaji, kuathiri uwezo wa kufanya kazi na kuipelekea Serikali kugharamika katika kuwatibu waathirika wa dawa hizo thakili. Kamati inasisitiza wananchi wote, vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa kijamii na viongozi wa dini kushirikiana kwa pamoja katika kukabiliana na janga hili la dawa za kulevya.

## Ofisi ya Rais – Ikulu (ORI)

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa bajeti ya Ofisi ya Rais – Ikulu (ORI), michango ya Wajumbe wengi iligusia suala la kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa upatikanaji fedha kwa ajili ya utekezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa kuzingatia hadhi ya Ofisi hii, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha miradi yake ya maendeleo haikabiliwi na uhaba wa fedha kwa kuweka mkakati maalum wa utoaji wa fedha kwa wakati ili kukamilisha miradi katika muda uliyokusudiwa. Ili kuweza kuutekeleza ushauri huu, Serikali inapaswa kuweka mipango ya matumizi inayotabirika ili kuhakikisha kunakuwepo na mtiririko mzuri wa fedha za miradi ya maendeleo husuan ya Ofisi maalum kama hii.

## Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (ORTMSMIMSMZ)

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa michango iliyochangiwa kwa msisitizo katika Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ mkubwa ni kuwepo kwa changamoto ya kutolipwa kwa wakati kwa Wakala wa Ulinzi baada ya kutoa huduma kwa taasisi za Serikali na binafsi. Hali hii imeathiri mapato ya Wakala na kusababisha ucheleweshaji wa mishahara kwa watendaji wake licha ya Wakala kutoa huduma kwa ufanisi. Kwa kuzingatia umuhimu wa huduma zinazotolewa na Wakala wa Ulinzi, Kamati inaishauri Serikali kuzihamasisha taasisi zinazodaiwa kulipa madeni yao kwa wakati. Vilevile, Wakala wanashauriwa kuandaa mkakati wa kufuatilia na kufanya mazungumzo na taasisi husika ili kuweka utaratibu wa ulipaji wa madeni hayo kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi waliipongeza Serikali kwa kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha kwa Unguja na Pemba. Kukamilika kwa mradi huu, kutaimarisha kwa kiasi kikubwa mazingira ya kazi na kuwawezesha masheha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha ofisi hizo zinawekwa makatibu wa masheha ili kusaidia katika utoaji wa huduma, hasa pale masheha wanapokabiliwa na dharura au kutokuwepo ofisini.

## Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (ORKSUUB)

**Mheshimiwa Spika,** Suala la maslahi ya watendaji wa Baraza limesisitizwa sana na Wajumbe walipokuwa wakichangia Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Licha ya kuyafanyiwa kazi mapendekezo ya posho, Kamati pia inaungana na Wajumbe kuisisitiza Serikali kulimaliza suala hili kwa kuyafanyia kazi mapendekezo ya mishahara ya watendaji wetu hawa kwani si jambo la upendeleo bali ni

haki yao kwa mujibu wa Muundo wa Utumishi (Scheme of Service) ambao umeidhinishwa na Serikali kupitia Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Watendaji hawa wa Ofisi ya Baraza wanastahili kutambuliwa kwa upekee wa kazi zao na kulipwa maslahi stahiki yanayoendana na dhamana kubwa wanayoitekeleza. Utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Wawakilishi, kama ulivyoainishwa katika Katiba, unasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kuongeza motisha na ari ya kufanya kazi, Watendaji hawa wanastahiki kupewa maslahi yao kwa mujibu wa viwango vinavyostahiki katika muundo wa utumishi wa Baraza. Aidha, taasisi nyingi tayari zimeshafanyiwa kazi mapendekezo ya mishahara na maposho kulingana na mapendekezo ya miundo ya mishahara na maposho ya taasisi husika. Hivyo, ni muhimu kuharakishwa zoezi la kupatiwa stahiki zao ili kuimarisha maslahi ya watendaji hawa kwa kuzingatia mchango wao mkubwa katika kuendesha shughuli za Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa na Wajumbe ni suala la maslahi ya walimu wa madrasa. Kwa kuwa madrasa ni suala muhimu katika malezi ya vijana wetu kidini na kijamii, Kamati inaishauri Serikali kuanza kulichukuliwa hatua za dhati suala hili la maslahi ya walimu wa madrasa kwa kuanza kufanya tathmini kuhusu hali halisi ya walimu wa madrasa, ikiwa ni pamoja na idadi yao, mahitaji yao, na mazingira ya kazi, ili kuweka msingi wa sera ya kitaifa ya kuwatambua na kuwahudumia na hatimae kuweza kutolewa malipo kwa walimu wa madrasa kwa utaratibu rasmi na endelevu. Aidha, Serikali inapaswa kuimarisha Baytul-Maal kimuundo na kifedha, na kuwe na uwazi zaidi katika uendeshaji wake kwani inaweza kutumika kama chanzo cha mapato kusaidia malipo ya walimu hawa.

## Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji (ORKUU)

**Mheshimiwa Spika,** Suala la upatikanaji wa ajira za staha ni miongoni mwa masuala yaliyowekewa msisitizo mkubwa na Wajumbe katika mjadala wa bajeti ya Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji imepanga kuratibu upatikanaji ajira 20,000 ndani na nje ya nchi kama sehemu ya juhudi za kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana. Kamati inaunga mkono hatua hiyo sambamba na kuishauri Serikali kuhakikisha ajira hizo zinakuwa na mikataba inayozingatia misingi ya heshima, utu na haki za mfanyakazi.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (WHVUM)

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wajumbe wengi wameipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kutekeleza vyema Programu ya Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo ambapo viwanja vya michezo vilivyomaliza kutengenezwa au kukarabatiwa vimekuwa vikitumika katika michezo mbali mbali. Kwa kuwa suala la uimarishaji wa michezo ni moja kati ya vyanzo vya upatikanaji wa ajira, Kamati inaungana na Waheshimiwa Wajumbe kuipongeza Serikali sambamba na kuishauri kuwasisitiza wahudumu na watumiaji wa viwanja hivyo kuvitunza ili viweze kudumu na kutumika kwa muda mrefu ili kuleta tija iliyokusudiwa.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale (WUMK)

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini limepokelewa kwa mtazamo chanya na limechangiwa kwa msisitizo na Waheshimiwa Wajumbe wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii. Ongezeko hili lina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa

Zanzibar kupitia mapato ya moja kwa moja na upatikanaji wa ajira, hasa katika sekta ya huduma, biashara ndogo ndogo, na uwekezaji. Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuanzisha mfumo mpya wa kihesabu wa ***Tourism Satellite Account (TSA)***, ambao utasaidia kuonesha kwa usahihi mchango wa sekta ya utalii katika Pato la Taifa na kuwezesha maamuzi ya kisera yanayozingatia uwepo wa taarifa za kutosha. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utekelezaji kamili wa mfumo huu, kuimarisha mifumo ya kidijitali ya ufuatiliaji wa wageni, na kuwekeza katika tafiti na takwimu zinazohusiana na mwenendo wa soko la utalii. Aidha, Serikali ihakikishe kwamba taarifa hizi zinatumika kikamilifu katika kukuza sekta ya utalii sambamba na kuimarisha mapato ya sekta hii.

## Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto (WMJJWW)

**Mheshimiwa Spika**, Suala la uimarishwaji wa mabaraza ya watoto ambayo kwa sasa yanaishia katika ngazi ya Shehia ni miongoni mwa maeneo yaliyosisitizwa na Wajumbe kwa msisitizo pamoja na kuishauri Serikali kuandaa mikakati ya kuyainua mabaraza hayo na kufikia ngazi ya Mkoa. Kwa kuwa mabaraza hayo yalianzishwa ili kushirikisha watoto katika kupanga mustakabali wao, Kamati inaungana na hoja zilizotolewa na Wajumbe sambamba na kuishauri Serikali kuandaa mipango maalumu kuhusu mabaraza hayo ili kuwezesha ujengaji wa jamii bora kwa kuwapatia elimu kuhusiana na haki na wajibu wao, pamoja na uwezo wa kujenga kujieleza na kujilinda dhidi ya ukatili wa aina mbali mbali. Aidha, Kamati inatoa wito kwa wazazi kuwaruhusu na kuwasaidia watoto wao kushiriki katika mabaraza hayo kwani ni haki yao kushiriki na kushirikishwa kwenye masuala yanayowahusu mustakabali wa maisha yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine katika Wizara hii, Waheshimiwa Wajumbe waliipongeza Serikali kwa hatua ya kuongeza kiwango cha pensheni kwa wazee waliotimiza umri wa miaka 70, kutoka shilingi 20,000 hadi kufikia shilingi 50,000 kwa mwezi. Hatua hii inaonesha dhamira njema ya Serikali katika kuhakikisha ustawi na heshima ya wazee wetu ambao walitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Kamati inaungana na Waheshimiwa Wajumbe kutoa pongezi kwa Serikali kwa uamuzi huu, sambamba na kuishauri kuendelea kufanya mapitio ya kiwango hicho ili kiendane na gharama za maisha, kupanua wigo wa walengwa, na kuimarisha mifumo ya usajili na ulipaji ili kuhakikisha ufanisi, usahihi na uwazi.

## Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda (WBMV)

**Mheshimiwa Spika,** Suala la uimarishaji wa sekta ya viwanda vya ndani limechukua nafasi kubwa katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe, ambapo wameisisitiza Serikali kubuni mikakati thabiti ya kuimarisha maeneo ya viwanda na kuwawezesha wajasiriamali wazalendo kuzalisha bidhaa kwa kutumia malighafi zinazopatikana ndani ya nchi. Ili kufanikisha azma hii, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza na kutekeleza sera wezeshi za viwanda, ikiwa ni pamoja na kutoa vivutio kwa wawekezaji wa ndani, kupunguza gharama za uzalishaji kama vile umeme na usafirishaji, na kuimarisha miundombinu ya viwanda vidogo na vya kati (SMEs). Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha upatikanaji wa mitaji nafuu kupitia taasisi za kifedha, kuanzisha vituo vya ubunifu wa viwanda (industrial incubation centres), na kutoa mafunzo ya kitaalamu kwa wajasiriamali ili kuongeza thamani ya bidhaa na ushindani wa soko.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo lilichangiwa na Wajumbe wengi ni umuhimu wa kuimarisha miundombinu ya bandari ili kurahisisha na kuharakisha ushushwaji wa bidhaa, hususan bidhaa za chakula. Hatua hii ni ya msingi katika kudhibiti mfumko wa bei unaochangiwa na ucheleweshaji wa upakuaji wa mizigo kutoka katika meli. Kwa kuzingatia hilo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya bandari, ikiwemo kuharakisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bandari ya Mangapwani, ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kushushia mizigo, kuimarisha mifumo ya uagizaji na kutoa kipaumbele kwa bidhaa za chakula. Aidha, Kamati inashauri kuimarishwa kwa ushirikiano wa Serikali na sekta binafsi ili kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa bandari, sambamba na kuimarisha usimamizi wa bei za bidhaa muhimu sokoni.

### Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo (WKUMM)

**Mheshimiwa Spika,** Suala la uimarishaji wa zao la karafuu limechukua nafasi kubwa katika mjadala wa Wizara hii kutokana na umuhimu wa zao hilo katika uchumi wa nchi yetu. Wajumbe walisisitiza umuhimu wa Serikali kushirikiana na taasisi za kifedha ili kuwawezesha wakulima wa zao la karafuu, kuongeza uzalishaji wa miche bora, kupata pembejeo kwa wakati ili kuweza kuzalisha karafuu zenye ubora wa juu zinazokidhi mahitaji ya masoko ya kimataifa. Kwa kuzingatia umuhimu wa zao hilo katika uchumi wa Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kuweka msukumo mahsusi (incentive) utakaogusa moja kwa moja wakulima ikiwa ni pamoja na ruzuku ya pembejeo, huduma za ugani, na ununuzi wa miche ili kuinua tija, kuongeza kipato cha wakulima na kulipa kipaumbele zao la karafuu kama zao la kimkakati la taifa.

## Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (WAMM)

**Mheshimiwa Spika,** Michango ya Wajumbe wengi katika Wizara hii ilisisitiza suala la kuwepo kwa malalamiko ya kuchelewa kufanyiwa tathmini kwa wananchi waliopisha maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hususan kucheleweshwa kwa tathmini ya mali zao kama vile vipando na makaazi. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kusajili wathamini wengine wa ardhi, na ili kuweza kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kusajili wathamini wa ardhi wenye sifa stahiki na kuongeza rasilimali watu katika maeneo yenye utekelezaji wa miradi. Vile vile, Serikali inatakiwa kuweka utaratibu maalum wa muda wa kikomo wa kufanyika kwa tathmini, ulipaji fidia na kutoa mrejesho kwa wananchi, ili kujenga mazingira ya haki, uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa ardhi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa na Wajumbe ni kuwepo kwa migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiendelea kila siku kutokana na utekelezaji wa kusuasua wa taratibu za upimaji wa ardhi pamoja na uchelewaji wa uwamuzi kutoka kwa wahusika wa ufuatiliaji wa migogoro hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mamlaka zinazoshughulikia migogoro ya ardhi zinafuata kikamilifu na kwa haraka taratibu zilizowekwa kuhusu uhaulishaji wa ardhi ili kuepusha migogoro ya ardhi. Sambamba na hayo, Kamati inatoa wito kwa wananchi kufuata utaratibu wa kisheria katika uhaulishaji wa ardhi ili kuepuka migogoro katika siku za baadae.

## Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (WUMU)

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Wajumbe wengi wameomba kuongezwa kasi ya ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa barabara. Ili kuitatua changamoto

hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi na kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo, kwa kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa wakati, kuimarisha usimamizi kwa wakandarasi, pamoja na kuondoa vikwazo vya kiutaratibu vinavyochelewesha utekelezaji. Hatua hii ni muhimu ili kuimarisha huduma za usafirishaji zitakazochochea shughuli za kiuchumi na kuinua ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Suala jengine lililochangiwa na Wajumbe wengi ni kuwepo kwa changamoto ya kutokukamilika kwa zoezi la malipo ya fidia kwa maeneo ya Mradi wa Ujenzi wa Uwanja Mpya wa Ndege - Pemba. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa tathmini ya fidia kwa wananchi walioathiriwa na mradi inakamilishwa haraka. Aidha, malipo ya fidia yatolewe kwa wakati ili kuondoa malalamiko ya wananchi na kuruhusu utekelezaji wa mradi kuendelea kwa ufanisi. Kukamilika kwa zoezi hili kutaendelea kuimarisha uhusiano mwema kati ya Serikali na wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuongezeka kwa ajali za barabarani hususan zinazohusisha waendesha bodaboda, Wajumbe wengi waliweka msisitizo kwa Serikali kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha utoaji wa elimu ya usalama barabarani kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara, kuweka mikakati madhubuti ya ukaguzi wa vyombo vya moto, na kuhakikisha waendesha bodaboda wanapata mafunzo rasmi na leseni halali. Aidha, ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi, mamlaka za usafiri, na vyama vya madereva ni muhimu katika kudhibiti tatizo hili linaloathiri maisha na uchumi wa wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa ni kupewa kipaumbele cha ajira katika miradi ya maendeleo kwa vijana wa Zanzibar. Kamati inashauri Serikali kuweka mkazo katika kuhakikisha vijana wetu wanapewa kipaumbele cha ajira katika utekelezaji wa miradi ya

maendeleo, hasa ile inayotekelezwa katika maeneo yao. Hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana, kuongeza ujuzi kupitia ajira za muda na mafunzo kazini, pamoja na kukuza ushirikishwaji wa wananchi katika maendeleo.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wajumbe wengi walitoa pongezi nyingi kwa Serikali kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya elimu. Kamati inaungana na Waheshimiwa Wajumbe kuipongeza Serikali kwa juhudi hizo zinazoonesha dhamira ya dhati ya kuendeleza sekta ya elimu nchini. Aidha, Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kuwekeza katika sekta hii ili kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora itakayowawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya juhudi kubwa zilizofanywa na Wizara hii katika utekelezaji wa miradi mingi ya ujenzi wa skuli mpya za ghorofa lakini bado kumekuwepo na uhitaji wa kujengwa skuli mpya, kufanya ukarabati, kujenga madarasa na vyoo ili kufikia azma ya wanafunzi kwenda mkondo mmoja. Kamati inaishauri Serikali, kuendelea na mikakati ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu kwa kuweka kipaumbele kwa kuanza miradi katika yale maeneo yenye mahitaji zaidi. Aidha, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, Kamati inasisitiza kwamba suala la uimarishaji wa miundombinu ya elimu uende sambamba kwa kadri inavyowezekana na suala la upatikanaji wa walimu wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa ni kuwepo kwa changamoto ya kuchelewa kupata fedha za mkopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Wajumbe wengi walisisitiza kwamba fedha hizo ziwe zinapatikana kwa wakati kwani baadhi ya wanufaika wanasoma vyuo vya

nje ya Zanzibar tena baadhi yao ni watoto wa kike. Aidha, Kamati inaunga mkono hoja ya Serikali ya kuwataka wanufaika kufanya marejesho ya mikopo yao ili kuiwezesha bodi ya mikopo kuwapatia wanafunzi wengine.

**Mheshimiwa Spika**, Suala la kuchelewa kulipwa madeni ya posho za walimu pia limechangiwa na Wajumbe wengi. Kamati imefarijika na hatua ya Wizara ya Elimu kuanza kuwalipa walimu stahiki zao. Kamati inaishauri Wizara, kumaliza zoezi hili la malipo ya madeni ya nyuma sambamba na kujipanga kwa siku za baadae ili kusiwepo tena na mkusanyiko wa madeni.

## Wizara ya Afya (WA)

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi walipokuwa wanachangia bajeti ya Wizara hii waligusia suala la Serikali kuendelea na ujenzi wa vituo vya afya hususan katika maeneo yenye wakaazi wengi. Ili kufikia malengo ya utekelezaji wa ujenzi wa vituo hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuufanya mradi kuwa endelevu kwa kuendelea kujenga vituo hivyo vya afya kwa awamu kwa kuyapa kipaumbele yale maeneo yenye wakaazi wengi zaidi na yale ambayo huduma za afya zipo mbali zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa katika Wizara hii ni suala la Serikali kuongeza ufuatiliajin wa maradhi ya malaria. Licha ya Serikali kuwa na azma ya kuitokomeza kabisa malaria (free from malaria), Kamati inasisitiza hatua hizi kuchukuliwa kwa haraka ili tuweze kufikia malengo hayo na kuepusha hali ya kurudi nyuma tulipotoka kwani maradhi haya yasipodhibitiwa ni tishio si kwetu sisi tu bali pia kwa sekta ya utalii na uwekezaji kutokana na wageni wanaweza kupata hofu ya kuja katika nchi yetu.

## Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (WUBU)

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kukosekana kwa vifaa vya boti walizopewa wananchi ni miongoni mwa maeneo yaliyochangiwa na Wajumbe wengi katika Wizara hii. Kamati imefarijika na hatua iliyochukuliwa na Wizara ya kutoa vifaa vya boti 508 kati ya 527. Hatua hii ni kubwa, na Kamati inaipongeza Wizara kwa kuitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto hii.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo limechukua muda mkubwa wa Wajumbe walipokuwa wakichangia bajeti ya Wizara Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi. Ingawa suala hili la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi ni suala la kitaalamu linahitaji muda na umakini, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwazi na mawasiliano ya mara kwa mara kwa umma kuhusu hatua zilizofikiwa katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, kuimarisha mazingira rafiki kwa wawekezaji wa kimkakati bila kuathiri maslahi ya nchi, kujifunza kutoka nchi nyingine za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Madola ambazo zimefanikiwa kusimamia sekta ya mafuta na gesi kwa ufanisi, kwa lengo la kuepuka makosa yanayoweza kuathiri maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Uchumi wa Zanzibar unategemea sana sekta ya utalii, kilimo na uvuvi, Kamati inaisisitiza Serikali kuzifanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ulinzi wa mazingira ili kuepuka uharibifu wa ikolojia ya ardhi na bahari yetu.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini (WMNM)

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara hii Wajumbe walichangia kwa wingi pamoja na kuisisitiza Serikali kuendelea kuongeza kasi na juhudi za

kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inapatikana kwa uhakika katika maeneo yote ya nchi yetu. Ingawa Serikali imeshachukua hatua mbali mbali ikiwemo ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji na uchimbaji wa visima, ipo haja sasa Serikali kuelekeza nguvu zaidi katika kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa maji ili huduma hiyo iweze kuwafikia wananchi katika maeneo yote yaliyokusudiwa. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri ZAWA kutumia teknolojia ya ufuatiliaji wa mtiririko wa maji na kupunguza upotevu wa maji jambo ambalo itasaidia kuongeza ufanisi na kupunguza gharama. Aidha, Serikali iharakishe utayarishaji na matumizi ya ramani ya pamoja ya miundombinu ya chini ya ardhi ili kujua mahali mabomba ya maji, waya za umeme na mkonga wa mawasiliano ili kuepusha uharibifu wa miundombinu hiyo hususan wakati wa ujenzi wa barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi walitoa msisitizo mkubwa kuhusu umuhimu wa kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika. Ili tuweze kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika, Serikali inapaswa kuweka mkazo katika kutafuta vyanzo mbadala vya umeme. Hii itasaidia pia kuvutia uwekezaji. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha miundombinu ya usambazaji umeme ili kuepusha upotevu wa umeme na hitilafu za mara kwa mara.

## Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (ORFM)

**Mheshimiwa Spika,** Michango ya Wajumbe wengi katika Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango (ORFM) iliweka msisitizo mkubwa juu ya umuhimu wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kama nguzo ya msingi ya kujitegemea kifedha na kupunguza utegemezi wa misaada na mikopo ya nje. Sambamba na hilo, Waheshimiwa Wajumbe wametoa pongezi nyingi kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) – Zanzibar kwa kuonyesha ufanisi katika ukusanyaji wa

mapato iliyopelekea kuvuka malengo ya makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inayotegemea vyanzo vya ndani huwa na kinga madhubuti dhidi ya athari za mabadiliko ya kiuchumi duniani, kama vile kupungua kwa misaada, masharti ya wakopeshaji wa kimataifa au mabadiliko ya viwango vya riba. Mapato ya ndani huipa Serikali uwezo wa kugharamia huduma za msingi bila kutegemea misaada au mikopo kutoka nje. Hali hii huimarisha mamlaka ya nchi katika kupanga na kutekeleza vipaumbele vyake vya maendeleo kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi, na sio masharti ya wafadhili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na ili kufikia ulipaji wa kodi kwa hiari Zanzibar, ni muhimu kujenga mazingira ya ushikiano, uaminifu na urahisi wa kulipa kodi hizo. Elimu endelevu kwa walipakodi na wananchi kwa ujumla, kuongeza uwazi katika matumizi ya kodi hizo, kuwepo mifumo rafiki ya ulipaji kodi, na ushirikiano wa kijamii ni nguzo muhimu zitakazojenga utamaduni wa ulipaji wa hiari wa kodi kwa maendeleo ya kweli ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa na Wajumbe wengi ni umuhimu wa kuimarisha utaratibu wa kufanya uchunguzi wa kitaalamu na wa kina (due diligence) unaofanywa na bodi ya zabuni kwa wakandarasi na watoaji wa huduma kwa Serikali ili kubaini usahihi wa taarifa za wazabuni, pamoja na kufanya tathmini ya kina ya uwezo wao wa kutekeleza kazi walizoomba, ili kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi sahihi.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufanikisha uchunguzi wa kina wa wazabuni si tu kwamba ni suala la kiufundi, bali pia ni msingi wa kuhakikisha uwajibikaji, ufanisi na kupatikana thamani ya fedha za umma. Serikali inapaswa kuwekeza katika mifumo, wataalamu na miongozo madhubuti ili kuimarisha mchakato wa uchunguzi wa kitaalamu na wa kina (due

diligence) kwa manufaa ya nchi yetu.

## HOJA ZA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la mwisho ambalo Kamati yangu ya Bajeti imeliona ilisisitize kutokana na umuhimu wake na kutokana na kuchangiwa na Wajumbe wengi katika kila mjadala wa bajeti ya Wizara, ni suala la pongezi nyingi na za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini, thabiti na wenye maono ya mbali. Kamati inaungana kikamilifu na Waheshimiwa Wajumbe hao kumpongeza, kuonyesha shukrani na kuthamini juhudi za Mheshimiwa Rais hususan katika maeneo mawili ambayo Kamati imekuwa ikiyafanyia kazi katika utekelezaji wa majukumu yake. Maeneo hayo ni utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani. Katika maeneo haya, Kamati imeshuhudia upatikanaji wa mafanikio makubwa na kufikia hatua ya kuvuka malengo yaliyowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muktadha huu, Kamati imebaini kwamba uongozi wa Mheshimiwa Rais si tu umedhihirisha dhamira ya kweli ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa ufanisi, bali pia umeweka msingi imara wa kujenga Zanzibar mpya, yenye uchumi thabiti, huduma bora, na matumaini kwa vizazi vijavyo.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, napenda kuchukua fursa hii kuitanabahisha Serikali kwamba michango na hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa Wajumbe wamezitoa hazikuwa na dhamira ya kuikwamisha Serikali, bali ilikuwa na lengo la kuikosoa na kuishauri Serikali ili ziweze kurekebishwa na hatimae kuzifanya bajeti za Wizara na Serikali ziwe bora zaidi. Aidha, nawanasihi Mawaziri wote kwamba yale

muliyoyaahidi kuyachukua na kuyafanyia kazi, mutekeleze ahadi hizo kwa vitendo ili tija na ufanisi upatikane katika utekelezaji wa bajeti zetu. Jambo hili litalipa heshima kubwa Baraza na Serikali kwani Wajumbe wametumia muda mwingi kujadili na kutoa ushauri.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii pia kwa mara nyengine kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Hotuba hii kwa niaba ya Kamati yangu ya Bajeti. Sambamba na hilo, nawapongeza Mawaziri wote kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti za Wizara zao. Vilevile, natoa pongezi za dhati kwa Wajumbe wote Baraza kwa michango yao katika mijadala ya bajeti hizo. Michango yao kwa kiasi kikubwa imesaidia kuimarisha bajeti hizo, na hatimae kufanikisha kupitishwa zikiwa bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunikisikiliza kwa umakini mkubwa. Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

…………………………

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**